# ASUMBI GIRLS HIGH SCHOOL

# MUHULA WA 2 – DESEMBA 2021

# KIDATO CHA 4

# KISWAHILI KARATASI YA 3

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI KISWAHILI KARATASI YA TATU FASIHI**

1. a) i) Ni maneno yake Mwangeka (uk49.)
   ii) Anamwambia Ridhaa
   iii) Wamo katika uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Rubia.
   iv) Ni baada ya kuyakumbuka maneno ya Tila kuwa haifai kucheza na uwezo wa vijana katika jamii. (4 x 1 = 4)

   bi) Tashibihi – wao ni kama nanga.
   ii) Jazanda – merikebu inasimamia taifa la Wahafidhina.
   iii) Taswira – Picha ya merikebu inayozamishwa. (2 x 2 = 4)

   c) Jinsi vijana walizamisha merikebu ya Wahafidhina.
   i) Genge la wavulana watano linawabaka Lime na Mwanaheri kwa kukisia kwamba wazazi wao hawakuchangia uchaguzi wa Mwanzi.
   ii) Wanazorotesha usalama kwa kumvamia Subira na kumkata kwa sime kwa kumdhania kuwa hakumpigia kura Mwanzi.
   iii) Vijana wanawavamia abiria barabarani wakiongozwa na kijana aliyekuwa amevaa shati lenye maandishi “Hitman” na kuwachomea ndani ya magari.
   iv)Wanayachoma magari barabarani.
   v) Sauna anaiba watoto wake Lunga-Dick na Mwaliko na kuwatenga na dada yao Umu.
   vi) Pete anameza vidonge ili kuavya kitoto chake cha pili ila hakufanikiwa.
   vii) Zohali anajiingiza katika mapenzi na kupata mimba akiwa kidato cha pili.
   viii) Wanawe Kiriri wanakataa kurudi nyumbani- Kutoka ughaibuni walikoenda kusoma.
   ix) Vijana wanamdhalilisha Mwekevu baada ya kuibuka mshindi katika uchaguzi.
   x) Kipanga anaachia masomo kidato cha pili na kuanza kunywa kangara – ananusurika kifo.
   xi) Wanafunzi shuleni – wanakomsea Ridhaa- wanaendeleza ukabila dhidi ya wanafunzi walowezi.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

xii) Vijana wanapokea hongo kutoka kwa wanasiasa kama papa ili wawachague, hivyo kuimarisha uongozi mbaya.
xiii) Vijana wasichana wanajifungua watoto na kuwatupa kwenye majaa ya taka kama yule aliyeokolewa na Neema.
xiv) Wanavunja sheria kwa kuandamana huku wamebeba picha za Mwanzi na kumhimiza atawale ingawa alikuwa ameshindwa n.k. (12 x 1 = 12)

2. a) (uk.83)
- msemaji ni babu
- anamwambia Majoka
  Wako katika ambulensi
  -Majoka anadhani daktari wake ni babu yake anapoongea naye akipelekwa hospitalini. (4×1=4)

b) Jazanda – chombo na rubani inalinganishwa na nchi na kiongozi.(alama 2 x 1 = 2)

c) Msemewa ni Majoka.
- Anawaua wapinzani wake.
- Anawafunga watetezi
- Anatumia wahuni kutisha wapinzani.
- Anaamuru polisi kuwapiga risasi raia. (alama 4 x 1 = 4)

d) Mambo yanayokwaza usawa:
i) Ubabedume
ii) Unyakuzi wa ardhi
iii) Ukatili
iv) Mauaji
v) Unyanyasaji
vi) Ufisadi
vii) Uongozi mbaya.
(viii) uharibifuwa mazingira
(ix) kukubalia biashara haramu.
(x)matumizi mabaya ya vyombo vya dola.
(xi)upiro miongeni mwa viongozi
(xii) ukwere miongoni mwa viongozi.
(Zozote 10 x 1 = 10) (atoe maelezo mafupi)

3. a) Maudhui ya usaliti.
i) Kombe anamuunga mkono Majoka kisiasa lakini Majoka anashurutisha kufurushwa kwake kupitia kwa vijikaratasi vilivyosabazwa.
ii) Ngurumo alisoma na Tunu lakini anamsaliti kwa kumuumiza miguu.
iii) Majoka anawasaliti wafanyi biashara wa Sagamoyo kwa kumwaga kemikali katika soko lao.
iv) Majoka anasaliti juhudi za kuhifadhi mazingira kwa kufungulia biashara ya ukataji miti.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

v) Mkuu wa polisi Kenga anamsaliti Majoka kwa kumtoroka hali ya kisiasa ilipokuwa mbaya.
vi) Raia wa Sagamoyo wanasaliti wajibu wao wanapoendelea kumuunga mkono Majoka "dikteta".
vii) Shule ya Majoka and Majoka Academy inasaliti wanafunzi kwa kuwaruhusu kutumia mihadarati.
viii) Ngurumo anamsaliti Boza kwa kushiriki mapenzi na Asiya mkewe.
ix) Majoka anasaliti raia kwa kufunga soko la Chapakazi.
x) Majoka anasaliti wapiganiaji haki kwa kumuua Jabali mpinzani wake.
xi) Kenga anawasaliti Wanasagamoyo kwa kuunda genge ambalo lilizorotesha usalama.
xii) Majoka anasaliti Chopi kwa kupanga na Kenga ili auwawe licha ya kwamba alikuwa amemtumikia kwa muda mrefu.
xiii) Majoka anawasaliti raia kwa kuchukua mikopo na kuitumia kwa mirandi isiyo wanufaisha.
xiv) Serikali inamsaliti Ashua kwa kukosa kumwajiri licha ya kuwa amehitimu.

(zakwanza 10 x 1 = 10)

b) Jazanda

i) Rubani – Viongozi wa jimbo la Sagamoyo
ii) Kigogo – kiongozi wa Sagamoyo
iii) Keki ya Uhuru – Raslimali za nchi
iv) Kutoa tonge mdomoni – tonge la Husda – Majoka ambaye ni mumewe.
v) Kuku – Sudi ambaye ni mumewe Asha
vi) Chatu mmoja kutolewa kafara – chatu ni Sudi au Tunu auwawe.
vii) Majoka kutotumia bomu kuua mbu – hangetumia nguvu nyingi kuua Tunu. – anauwezo.
viii) Chatu kumaanisha watu wanaotekeleza mauaji wanapoambiwa na kiongozi – akina Ngurumo.
ix) Majoka kumshauri Sudi anawe mikono ili ale na watu wazima – akubali kuchonga kinyago ili Ashua aachiliwe.
x) Majoka kuwa katika chombo cha safari ya jongomeo – uongozi wake unakaribia kuisha.
xi) Kisima kuingiwa na paka na maji hayanyweki – mambo yameharibika Sagamoyo.
xii) Chombo cha Majoka kwenda kinyumenyume – Majoka haleti maendeleo Sagamoyo.
xiii) Marubani wasioendesha vyombo vyao vizuri – Viongozi wabaya
xiv) Husda anafananishwa na chui anayeishi ndani ya ngozi ya kondoo – hampendi Majoka - unafiki
xv) Hashima anamuonya Tunu asijipeleke kwenye pango la nyoka – kujitia kwenye hatari
xvi) Tunu anadai moto umewaka – harakati za kumng'oa Majoka zimeanza.
xvii) Sumu ya nyoka – dawa za kulevya.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

xviii) Kanga – Majoka – mumewe Husda
(za kwanza 10 x 1 = 10)

4. **USHAIRI**

a) Bahari nne

viii) Ukara – vina vya mwisho vina urari
ix) Mathnawi – vipande 2 ukwapi na utao katika kila mshororo
x) Tarbia/unne – mstari minne kwa kila ubeti
xi) Kikwamba – neno (naja) limeanza mshororo katika kila ubeti (4 x 1 = 4)

b) Lugha tutumbi

-Ninarudi hapo kwetu na nitakuwa hapo
-Hata nikiambiwa pananuka nitakaa tu
-Siendi pengine hivyo narudi hapo tu
-Nyundo ninakuja misumari jihadharini (4 x 1= 4)

c) Amekomaa – anasema amekomaa kuliko mwanzo (2 x 1 = 2)

d) Mzalendo anayeipenda nchi yake – hata kama pananuka atarudi tu
Anataka kurudi kufaa nchi yake. (kutaja alama 1, kueleza alama 1 = 2)

e) i) mwando – mwanzo
ii) Ningambwa – ningaambiwa (2 x 1 = 2)

f) Uhuru wa kishairi

i) Inkisari -ametumia ritifaa – 'mi – mimi
-'tarudi – nitarudi
- 'mekomaa – nimekomaa
-'tafiya - nitafia

ii) Tabdila - Sitapakimbiya – sitapakimbia

- tafiya – tafia

iii) kilahaja – ndiyani – njiyani

-Mwando – mwanzo
-Ningaambwa – ningaambiwa.

v) kuboronga sarufi – naja kwetu mzalendo – mzalendo ninakuja/naja kwetu

- kwetu 'mi nakutamani – ninatamani kwetu

- kulo na mwingine uhondo – kuna uhondo mwingi (2x2=4)

g) Wananchi wa kwao hasa waliomtendea maovu (ubeti wa mwisho) (2 x 1 = 2)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

5. a) ukabila (1 x 1 = 1)

b). dhamira i) kueleza jinsi nchi yetu ilivyokubwa na ukabila
ii) Athari zinazotokana na ukabila(2 x 1 = 2)

c) Muundo
i) beti tano
ii) idadi tofauti ya mshororo katika kila ubeti
iii) idadi tofauti ya mizani katika kila mshororo
iv) idadi tofauti ya vipande katika kila mshororo(4 x 1 = 4)

d) ubeti wa nne – tutumbi
Tuipende nchi yetu na tusaidie wanaohitaji usaidizi wetu. Tukumbuke kuwa nyumbani ni nyumbani hatakama haliyake ni gani. Ni tabia mbaya kueneza ukabila katika nchi yetu kwa sababu ni aibu kwa mtu kumtukana mama yake. (4 x 1 = 4)

e) Mbinu mbili
i) Takriri – ukabila ukabila
ii)Balagha – Wanasiasa matapeli?
iii)Istiari – ukabila ni shetani. (2 x 2 = 4)

f) Njia ya kumaliza ukabila
i) Kuhakikisha kuwa kila jamii imeshirikishwa katika uteuzi wa kiserikali.
ii) Kuanzisha kampeni za kumaliza ukabila.
(1 x 1 = 1) (atoe maoni yake)

g) Uhuru wa Ushairi
i) inkisari – waumiza – unaumiza
ii) kuboronga sarufi – wasituhadae watu hawa – watu hawa wasituhadae.
iii) Tabdila – tuangamiye – tuangamie
iv) msamiati kale/lahaja – Jalali – Mungu, Nina – Mama (zozote 4 x 1 = 4)

6. a)- Maneno ya Sara
-"uzugumzi nafsia"
- akijiambia anarejelea alivyobakwa na jitu
-Tayari alikuwa mjamzito kutokana na ubakaji. 4x1=4

b) mbinu za lugha
i) takriri – kwa nini kwani nini
ii) balagha – kwa nini hasa?
iii) uzungumzi nafsi – wa Sara (2 x 1 = 2)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

c) sifa nne za Sara
i) mwenye mapenzi ya dhati
ii) mwenye utu
iii) mwoga
iv) mwenye busara
v) mkakamavu
vi) msamehevu.
(lazima atoe maelezo, lazima amtaje Sara, za kwanza 4 x 1 = 4)

d. Athari za ubakaji.
i) Sara anahisi mdidimo na mkadamizo wa kiwiliwili chake.
ii) ujauzito
iii) kuvunjwa ujana jike.
iv) kuharibiwa maisha.
v) Aibu na kudunishiwa na wandamu wenzake.
vi) kutengwa na wanajamii.
vii) Sara anaona laana na masumbuko kutoka kwa kila mtu aliye karibu naye.
viii) kilio na maombolezo katika familia.
ix) uoga kwa babake – atakavyokejeliwa na jamii.
x) kufukuzwa shuleni na mwalimu mkuu.
xi) hisia za kujiua.
xii) wazo la kutoa mimba – unyama
xiii) maafa – jitu linauwawa na wanakijiji.
(za kwanza 10 x 1 = 10) (lazima atoe maelezo mafupi na mifano kutoka kwa hadithi husika.)

7. a) Mapenzi ya kifaurogo
i) malezi duni – Dennis alalelewa katika mazingira ya kimaskini
ii) kuishi kwa majuto – Dennis anaishi kujihurumia
iii) kuaibishwa – Dennis anaaibishwa na Dkt Mabonga.
iv)upweke – Dennis anakumbuka wenzake wanavyojigamba.
v) Maisha duni chuoni – Dennis anaishi kwenye chumba kisicho na vitu vya dhamani.
vi) kupuuzwa – Dennis anapuuzwa na wachapishaji vitabu.
vii) kushindwa kukidhi masilahi ya kibinafsi.
viii) Dennis anakosa chakula akiwa chuoni.
ix) kulazimishiwa mapenzi – Dennis analazimishiwa mapenzi na Penina
x) kuishi maisha ya utegemezi – Dennis anamtegemea Penina.
xi) Ukosefu wa ajira – Dennis anaishi kipindi kirefu bila ajira.
xii) kusalitiwa kimapenzi – Dennis anasalitiwa na Penina baada ya kukosa kazi.
(zozote 8 x 1 = 8)

b) Masharti ya kisasa

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

i) kuhangaika kutafuta mapenzi- Dadi anahangaika akimtafuta Kidawa

ii) Kuadhibiwa kimapenzi – Dadi anapewe masharti magumu na Kidawa

iii) Wasiwasi katika ndoa – Dadi anaishi kwa wasiwasi kwa kudhania kuwa mkewe anamwendea kinyume.

iv) Kudhibitiwa na mke – Dadi alazimika kufanya kazi za nyumbani ambazo hazimwafiki mwanamume.

v) Dhihaka ya majirani – Dadi anadhihakiwa na Bii Zuhura.

vi) Kupata majeraha ya mwili – Dadi alianguka na kupoteza fahamu pale shuleni akichunguza kama kidawa ana uhusiano wa kimapenzi na mwalimu mkuu. (zozote 6 x 1 = 6)

c) Ndoto ya Mashaka

i) upweke na ukiwa wakuvunjikiwa na ndoa. – Mashaka anaingiwa na upweke baada ya ndoa yake kusambaratika.

ii) Uyatima – Mashaka alipoteza wazazi wake akiwa mtoto mdogo.

iii)kazi ngumu – Mashaka analazimika kufanya kazi ngumu shambani.

iv)kukosa Elimu – Mashaka hakuweza kuendelea na masomo yake.

v) Malezi duni – Mashaka alilelewa na Bi. Kidebe aliyekuwa maskini.

vi) Pingamizi za familia katika suala la mapenzi – Mapenzi kati ya Mashaka na Waridi yalipingwa nafamilia ya Mzee Rubeya.

(zozote 6 x 1 )(mtahini akadirie jibu la mwanafunzi katika swali hili. )

8. (a) ( i) Ulumbi 1 x 1

(ii)- matumizi ya lugha yenye mnato/tamathali za usemi – mwacha mila ni mtumwa

- Taswira – ya urembo, misuli tinginya.

- Takriri – turathi zetu, turathi zetu.

- Kusema moja kwa moja mbele ya hadhira – nawasabahi.

- Anafahamu hadhira yake (utamaduni)

(za kwanza tatu 3 x 1 = 3)

b) Sifa zisizojitokeza katika kifungu

i) kupanda na kushuka kwa toni.

ii) kupaza sauti.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

iii) kuvaa maleba maalum.

iv)matumizi ya viziada lugha.

v)miondoko jukwaani

vi) kutua kidrama katika maongezi

vii) huenda akaimba, akauliza maswali, akaulizwa maswali na hadhira yake

(za kwanza 5 x 1 = 5)

c)

i) Asasi ya ndoa – mijadala ya mahari, utatuzi wa migogoro au kuchumbia

ii) Maabadini

iii) mahakamani

iv) Siasani

v) Asasi ya elimu

vi) Muktadha wa upatanishi

(za kwanza 4 x 1 = 4)

d)

i) Inaenzi uzee

ii) inaenzi urembo

iii) wavulana wanastahili kuwa na nguvu.

iv)utamaduni unaenziwa

v)Niwafugaji wa nyuki

(za kwanza 4 x 1 = 4)

e)

i) kutumia vinasa sauti

ii) kutumia kanda za kunasa video

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

iii) kuandika mazungumzo ya mtendaji

iv) kusikiliza kwa makini.

(za kwanza 3 x 1 = 3) (mtahiniwa atoe maelezo mafupi katika swali hili. Mtahini akadirie jibu la mwanafunzi.)

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/